# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

SHULE YA SEKONDARI MAKUZANI,
S.L.P 465,
**SUMBAWANGA**
TAREHE ……………………

Kumb. Na. MSS/VOL 1/1/06

MWANAFUNZI …………………………………………………………………………………………
S.L.P ……………………………

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MAKUZANI WILAYA SUMBAWANGA MKOA WA RUKWA MWAKA 2021**

## 1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021 Shule ya sekondari Makuzani ipo umbali km 35 kusini mwa halmashauri ya sumbawanga. Mhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe ………………….., Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe ………………. Na mwisho wa kuripoti ni tarehe ……………..

## 2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1. Sare ya shule

**A: WAVULANA**

i. Suruali mbili zaheshima moja rangi ya kaki na nyingine kijani kibichi naambatanisha na mfano wake
ii. Mashati meupe mawili yenye mikono mifupi
iii. Viatu pea mbili vya ngozi nyeusi na vyenye visigino vifupi na vya kamba
iv. Soksi rangi nyeusi jozi mbili au zaidi.
v. Sweta rangi ya bluu

**B.WASICHANA**

i. Sketi mbili za malinda ,moja rangi ya kaki na nyingine kijani kibichi
ii. Mashati mawili ya mikono mifupi
iii. Viatu pea mbili vya ngozi nyeusi na vyenye visigino vifupi na vya kamba
iv. Soksi ndefu rangi nyeupe jozi mbili
v. Sweta rangi ya bluu
vi. Magauni mawili ya kuvaa wakati wa kazi(shamba dress)dark blue)

C: Kwa atakayetaka kuvaa hijabu ifanane na sare za shule

**D: SARE ZA MICHEZO**

i. Bukta moja ya michezo rangi ya bluu kwa wavulana
ii. Sketi moja ya bluu kwa wasichana.
iii. Viatu vya raba rangi nyekundu kwa wote
(iv) Tirshit ya rangi ya blue.

**2.2 MAHITAJI MENGINE**

i. Daftari kumi kubwa za masomo yote (**counter book**)
ii. Mkebe wa hesabu kalamu za wino bluu au nyeusi na penseli za kutosha

iii. Aje na dictionary oxford **(kiingereza Kiswahili)**kwa ajili ya kujifunza lugha ya kiingereza.

iv. Mwanafunzi anatakiwa awe na jembe ,fyekeo na fagio (la chelewa) kwa ajili ya shamba na usafi wa mazingira.

E; Kuna upungufu mkubwa wa viti na meza hivyo kila mwanafunzi anatakiwa kuja na kiti na meza vya chuma kipimo cha viti na meza kinapatikana hapa shuleni

2.3 Huduma ya chakula inapatikana hapa shuleni kwa kuchangia gunia moja la mahindi na maharage debe moja na nusu kwa muhula na fedha taslimu **sh.40,000 elfu** kwa ajili ya kulipa wapishi sukari mafuta n.k.

**Kwa wanafunzi wa hosteli waje**

i. Godoro moja dogo la saizi mbili na nusu
ii. Chandarua cha pembe nne
iii. Sanduku la kuhifadhia vifaa vyake pamoja na kufuli
iv. Vyombo vya kulia chakula sahani,bakuli,kikombe n.k
v. Mashuka mawili rangi ya bluu na blanketi nzito kuna baridi
vi. Ndoo mbili ndogo zenye ujazo wa lita kumi ndoo moja ya kuogea na nyingine kwa ajili ya jikoni
vii. Matibabu ya mwanafunzi ni ghalama za mzazi

## 3. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu ya elimu na 25 ya mwaka 1995 aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya elimu na mafunzo ya ufundi yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya waziri mkuu OR-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu.Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na u tapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi wazazi wafanyakazi wote wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana ratiba ya shule ni lazima
c) Kushiriki kwa kufanya maandalizi ya jioni (preparation)
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako katika shule hii
f) Kutunza usafi wa mwili ,mavazi na mazingira ya shule
g) Kuvaa sare ya shule wakati worte unapotakiwa
h) Kuzingatia ratiba wakati wote na
i) Kutunza mali za umma

NB: Mwanafunzi alete miche mitatu ya miti (mikaratusi) ambayo atapanda na kutunza hadi atakapohitimu kidato cha nne

3.2 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa na kusimamishwa shule

a) Wizi
b) Uasharati na ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi cocaine mirungi kubeli n.k
e) Kupiga na kupigana
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
g) Kuzalau bendera ya taifa

h) Kuwa mjamzito/ kupata mimba
i) Kuoa /kuolewa
j) Kugoma ,kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
k) Kukataa adhabu kwa makusudi
l) Kuwa na simu ya mkononi

4. Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi/mzazi/mlezi

a) Medical examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospital ya serikali. Form hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
b) Form ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria ,kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa shuleni.

5. tafadhari soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu .

**KARIBU SANA KATIKA SHULENI HII**

.............................................................

A. AMANYISYE
MKUU WA SHULE
SIMU .0757494737/ 0784767858

THE HEADMAS[illegible]
[illegible]NI S[illegible] [illegible]DARY SCHO[illegible]
[illegible]